

SHUGHULI ZA KISWAHILI

GRADE 3 - 2020

Jina

Jinsia: Mvulana

Msichana

Jina la shule

Mwalimu ajaze mjalizo baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi.

	Swali la 1	Swali la 2	Swali la 3	Swali la 4
Idadi ya alama	15	5	20	10
Alama sahihi				

1. **KUSOMA**

Soma hadithi hii kwa sauti (Alama 15)

Maneno ya mwalimu wetu yametusaidia sana. Mimi na rafiki yangu tumekuwa tukifuata kila jambo tunaloambiwa na mwalimu. Kwa sababu hiyo tumejipata tukifanya vizuri katika masomo yetu na kuwa na adabu.

2. **UFAHAMU**

1. **Soma hadithi hii kisha ujibu maswali yafuatayo (alama 5)**

Siku ya michezo tulienda uwanjani kucheza. Mimi nilienda kuushangilia mchezo wa kandanda. Mimi sikuwa nimejua kuwa mchezo wa kandanda huwa na wachezaji kumi na mmoja kila upande. Nilijifunza mengi sana.

(a) Nyinyi huenda kucheza wapi? _____

(b) Mwanafunzi huyu alishangilia mchezo upi? _____

(c) Mchezo wa kandanda una wachezaji wangapi kila upande _____

(d) Andika michezo miwili unayoijua.

3. LUGHA


1. Andika sentensi hizi kwa wingi (alama 5)

- (a) Yeye atasoma _____
(b) Yeye atafanya kazi _____
(c) Yeye atarudi mapema _____
(d) Yeye atalima _____
(e) Yeye atashona nguo _____

2. Unda maneno kwa kutumia sauti hizi (alama 5)

- mw _____ mb _____
nd _____ nj _____
mt _____

3. Paka rangi sahihi za bendera yetu(alama 5)



4. Andika kwa maneno (alama 5)

- 56 _____
60 _____
85 _____

- 91 _____
73 _____

4. KUANDIKA (Alama 10)

Andika sentensi tano kuhusu 'shule yangu'.

Jumla (alama 50)

